Sikiliza Na Uelewe

(Hearken And Understand)

na

Alex S. Silvester

Sikiliza Na Uelewe

(Hearken And Understand)

na

Alex S. Silvester

Desemba 15, 2017

Sikiliza Na Uelewe

Yesu alitaka tuelewe ramani ya kanisa lake na jinsi ilivyo, sio tu hilo lakini pia alitutarajia kuelewa injili yake aliotuletea. Lakini kwa hakika wapo wale waliolikata na kumdhihaki na hawa ndio wale waliokataa kusikiliza ikihubiriwa. Anatuandaa na kutuandalia njia rahisi ya kuweza kumfikia na unaweza kukuta kwamba mwanadamu ni mwanadamu tu walimkataa na kufuata kisicho sahihi. Aliongea na watu binafsi na kwa upande mwingine, aliwatumia mitume wake kulitangaza. Baada ya mitume kufariki, walituachia nasi ili tuendelee kulihubiri na kuelewa ambacho Biblia inasema.

Tuangalie vifungu vinavyotusaidia kuelewa na kusikiliza ambacho anasema Bwana wetu:

"*Akawaita makutano tena akawaambia, nisikieni nyote na kufaham. Hakuna kitu kilicho nje ya mtu ambacho kikimwingia chaweza kumtia unajisi, bali vile vimtokavyo, ndivyo vimtiavyo unajisi yule mtu.*" (Marko 7:14-15). Mafarisayo bado walikuwa wakishikilia mila za wazee na hawakuelewa injili ilikuwa inahusu nini. Walidhani kwamba mtu anapokula chakula bila kunawa; inaweza kumtia unajisi. Lakini Yesu anawathibitishia kwamba hawako sawa pale anapowaambia kwamba kile kinachomtoka mtu ndicho kimtiavyo unajisi na siyo kimwingiacho. Waliendelea kumwabudu Mungu kwa hasara kwa sababu walikuwa wanafundisha maagizo ya wanadamu, hawakutaka kusikiliza na kusikia ambacho Mungu aliwataka wafanye. Mungu aliwataka waondoe mafundisho yote ya Musa ambayo yalikuwa ni maagizo ya wanadamu lakini hawakutaka kwa sababu hawakuelewa kwa hakika Injili.

Hili pia linaweza kututokea pale tunapoacha mfumo wa ibada na ramani ambayo Bwana wetu alituanzishia. Tunafuata maagizo ya wanadamu pale tunapoleta bisikuti na soda au pombe katika meza ya Bwana na tunapaswa kukumbuka kwamba hizi ni chachu. Lakini tunasahau pia kwamba Bwana wetu alipoanzisha meza yake kulikuwa na mkate usiotiwa chachu na uzao wa mzabibu. Kwa wale wanaojiita "Wakristo" wakati wanaleta vikombe vidogovidogo na kuvunja mkate katika vipande vidogovidogo na kuvipitisha kwa watu wakiita ni meza ya Bwana. Hawana tofauti na Mafarisayo na Waandishi waliojisifu kwamba walikuwa wanafanya jambo sahihi lakini siyo na nakumbuka ndugu Ellis alipokuwa akieleza kuhusu Yesu kuanzisha meza yake; aliita "Isiyochachwa" kama Biblia pia inavyoita. Na kutokana na ukweli huu mtume Paulo aliwasihi kanisa la Efeso kutenda vyema na kutafuta mwelekeo wa Mungu katika maisha yao. Tunaposhindwa kumtafuta

Mungu katika maisha yetu kwa miaka hii michache iliyobaki ulimwenguni tumepotea, lakini tunamtafutaje? Kwa kumsikiliza na kumwelewa kupitia neno lake.

"*Kwa sababu hiyo msiwe wajinga, bali mfahamu ni nini yaliyo mapenzi ya Bwana.*" (Efe. 5:17).

Mtume Paulo anamsihi Timotheo kwamba toka utotoni mwake aliyafahamu maandiko matakatifu, kwa nini? Kwa sababu alifundishwa na kushika na hivyo kuyaelewa vyema. "*Bali wewe ukae katika mambo yale uliofundishwa na kuhakikishwa, kwa maana unajua ni akina nani ambao ulijifunza kwao; na ya kwamba tangu utoto umeyajua maandiko matakatifu, ambayo yaweza kukuhekimisha hata upate wokovu kwa imani iliyo katika Kristo Yesu. Kila andiko yenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki; ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema."* (2 Tim. 3:14-17). Tunapaswa kuendelea katika mambo tuliojifunza kwa watu wa Mungu kama ndugu Ellis aliyekuja Afrika na kufundisha kwa hakika. Tunapaswa kusikiliza na kuelewa neno la Mungu ikiwa kweli tunataka kwenda katika sehemu aliokwenda kutuandalia. Tukilielewa, tunarekebishwa na kutuelimisha katika haki.

Mafarisayo na Waandishi walikuwa wasumbufu na watu wanaosababisha matatizo walidhani wako sahihi katika kila kitu walichokuwa wanafanya; na mara nyingi tunafanya makosa alafu tunajifanya kuwa sahihi. Yesu alionyesha kutokuelewa kwetu maandiko ni kwa sababu sisi ni wakaidi. Tunafanya juhudi katika kufanya mambo mengine vyema lakini tunasahau au hatutaki kusoma na kujifunza neno la Mungu kwa njia sahihi, hatumaanishi. Hata leo kuna "Wakristo" wanaofanya makosa pale wanapoanzisha matumizi ya vyombo vya mziki na kunena kwa lugha katika makusanyiko yao. "*Yesu akajibu akawaambia, mnapotea kwa kuwa hamyajui maandiko wala uweza wa Mungu. Kwa maana katika kiyama hawaoi wala hawaolewi, bali huwa kama malaika mbinguni.*" (Mat. 22:29-30). Kama nilivyosema hapo juu, tukifanya vitu kwa njia yetu na siyo kwa njia ya Mungu basi tunaingia katika matatizo; hiyo ni kumwabudu Mungu bure. "*Nao waniabudu bure wakifundisha mafundisho yaliyomaagizo ya wanadamu. Akawaita makutano akawaambia sikilizeni, mfahamu,*" (Mat. 15:9-10). Mkristo wa kweli ni lazima afundishe kama ilivyoagizwa katika kitabu kitakatifu (Biblia), na tunapaswa kumsikiliza na kumwelewa kupitia neno lake. Mtumwa lazima alisikize anachoambiwa na bwana wake au vipi kama akifanya ambacho hakuambiwa? Atakuwa amepotoka na anastahili adhabu. Na hicho ndio Mungu anaenda kutufanyia kama tusipowafundisha watu alichokisema katika Biblia na kuyafanya. Tuliwafikia kundi la watu fulani katika soko na tulipoanza kuongea nao

baadhi yao walikataa, wakisema “tumechoka na nyie watu” lakini kwa taratibu ndugu Caleb akawaambia watatu wao kukaa kama ikiwapendeza na tukajifunza nao. Kupitia uwezo wa Mungu watu wanne kutoka katika kundi hili walibatizwa. Nakumbuka tukio fulani baada ya Ellis kumaliza kufundisha somo Arusha, wawili waliitikia injili na wakataka kubatizwa na tukakodi Tax iliyotupeleka mtoni, na tulipofika mtoni hakukua na maji mengi; ilitubidi kuchimba ili maji yawe mengi na tukawabatiza. Ndugu zangu, lazima tufanye ambacho Mungu anatuagiza kufanya. Na tulichoambiwa kufanya ni kuwafundisha watu huko nje na pia sio wote watakubali baadhi watakataa. Lakini jukumu letu ni kuwaambia. “*Ingieni kwa kupitia mlango uliomwembamba; maana mlango ni mpana, na njia ni pana iendayo upotevuni, nao ni wengi waingiao kwa mlango huo. Bali mlango ni mwembamba, na njia imesonga iendayo uzimani, nao waionao ni wachache.*” (Mat. 7:13-14). Siyo kila mtu atakubaliana na tunachofundisha, lakini ni lazima tufundishe hata kama watakataa, hawa ndio wale wanaofuata njia pana. Yesu anatuambia ni kwa nini hatuelewi neno lake. “*Maana mioyo ya watu hawa imekuwa mizito, na kwa masikio yao hawasikii vema, na macho yao wameyafumba wasije wakaona kwa macho yao, wakasikia kwa masikio yao, wakaelewa kwa mioyo yao, wakaongoka nikawaponya.*” (Mat. 13:15).

Tunahitajika kuwa waungwana kama Waberoya; “*Watu hawa walikuwa waungwana kuliko wale wa Thesalonike, kwa kuwa walilipokea lile neno kwa uelekevu wa moyo, wakayachunguza maandiko kila siku, waone kwamba mambo hayo ndivyo yalivyo. Basi watu wengi miongoni mwao wakaamini, na wanawake wa Kiyunani wenye cheo, na wanaume si wachache.*” (Mdo. 17:11-12). Tunapaswa kulipokea neno kwa utayari wa nia, na kuyachunguza maandiko kila siku na siyo kupokea kila upepo wa mafundisho unaovuma mbele yetu. Lazima pia tuwajaribu hao wanaodai kufundisha habari njema. Biblia inatuambia kuwajaribu na kuwapa changamoto wale wanaokuja kwetu lakini kumbe hawajui chochote. Najifunza kitabu cha Yohana kwa undani na itatoka hivi karibuni.

Alex S. Silvester